## HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 17/01/2022.**

**A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mh. | Baisa A. Baisa | - Kata ya kitama | Mwenyekiti |
| 2. | " | Juma L. Nangololo | - Kata ya Mndumbwe | M/Mwenyekiti |
| 3. | " | Katani A. Katani | -Mbunge Tandahimba | Mjumbe |
| 4. | " | Aidani Chipande | - Kata ya Tandahimba | " |
| 5. | " | Milembu A. Mkwahe | - Kata ya Chaume | " |
| 6. | " | Sabihi T. Mtima | -Kata ya Mkundi | " |
| 7. | " | Jamali M. Mtonya | -Kata ya Mchichira | " |
| 8. | " | Mohamed S. Namgugu | -Kata ya Mahuta | " |
| 9. | " | Haruna A. Mwaya | -Viti maalum | " |
| 10. | " | Rehema S.Liute | - Kata ya Luagala | " |
| 11. | Ndg: | Mussa Gama | - Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |

**B: WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg: | Ramadhani Mwita | - Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 2. | " | Raphael Mputa | - Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 3. | " | Francis T. Mkuti | - Katibu Tawala (W) |
| 4. | " | Jacob Haule | - Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 5. | " | Mwajuma Mniachi | - Afisa Mipango |
| 6. | " | James Lyimo | - Kaimu TEO Tandahimba |
| 7. | " | Rajabu Lwazi | - Kaimu TEO Mahuta |
| 8. | " | Protas Muhanuzi | - Afisa Manunuzi na Ugavi (W) |
| 9. | " | Prisca Nsemwa | - Afisa Habari |
| 10. | " | William Kongola | - Mkaguzi wa ndani (W) |
| 11. | " | Mtaalam Mkana | - Kaimu Mifugo na Uvuvi(W) |
| 12. | " | Zuberi Sarahani | - Kaimu Mwanasheria (W) |
| 13. | " | Aloyce Massau | - Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 14. | " | Emmanuel John | - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 15. | " | Sostheness Luhende | - Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 16. | " | Martha Sinkamba | - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 17. | " | Issa Naumanga | - Afisa Kilimo Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 18. | " | Esmaily mbilinyi | - Mratibu TASAF |
| 19. | " | Violeth Mahembe | -Mratibu wa CHF |
| 20. | " | Temi Luther | - Kaimu Mhandisi Ujenzi(W) |
| 21. | " | John R. Mponda | - Kaimu Afisa Mazingira |
| 22. | " | Protas Lyapa | - Afisa TEHAMA |
| 23. | " | Hamisi Natenda | - Afisa Biashara |
| 24. | " | Juma A. Shoshi | - Afisa Utumishi |
| 25. | " | Dr. Ramadhani Msanzi | - Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 26. | " | Saumu B. Rashidi | - Kaimu Afisa Uchaguzi |
| 27. | " | Rosemary Mwalyagile | - Mratibu wa Vikao |
| 28. | " | Janeth Kawiche | - Mratibu wa Vikao |
| 29. | " | Nancy Lyimo | - Mratibu wa Vikao |

**MUHT.NA. 41/2022- KUFUNGUA KIKAO**
Katibu aliwasalimia wajumbe na kusema hiki ni kikao cha robo ya pili ambapo zitajadiliwa taarifa za Mwezi Oktoba - Disemba. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 5:37 asubuhi.

**MUHT.NA. 42/2022- KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**
Agenda kumi na moja (11) ziliwasilishwa mbele ya wajumbe wa kikao kwa ajili ya kuzipitia na kuziridhia ambazo ni:-

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuthibitisha Agenda za kikao
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 21/12/2021 na tarehe 22/12/2021
4. Taarifa ya Mapato na Matumizi Mwezi Disemba, 2021
5. Taarifa ya utekelezaji Miradi ya Maendeleo robo ya pili (Oktoba - Disemba 2021)
6. Taarifa ya utekelezaji kazi za idara robo ya pili (Oktoba - Disemba 2021)
   a) Idara ya Utumishi na Utawala
   b) Kitengo cha Manunuzi
   c) Kitengo cha Sheria
   d) Kitengo cha TEHAMA
7. Mpango wa Motisha wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba
8. Sera ya Mafunzo ya Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Tandahimba
9. Maombi ya kufuta deni la Tshs. 41,841,033.67/= ambazo ni fedha za mishahara ya watumishi waliofariki
10. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti
11. Kufunga kikao

**MUHT.NA. 43/2022- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 21/12/2021 na tarehe 22/12/2022.**
Muhtasari ya kikao cha tarehe 21/12/2021 na tarehe 22/12/2021 iliwasilishwa mbele ya kikao kwa ajili ya kuisoma na kuithibitisha. Wajumbe waliipitia Mihtasari hiyo na kuridhika na taarifa zilizoandikwa kuwa ni kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

**MUHT.NA. 44/2022- TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI DISEMBA, 2021**
Kaimu Mweka Hazina (W), aliwasilisha taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mwezi Disemba 2021, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:-

**SALIO**
Ilielezwa hadi tarehe 01 Disemba, 2021 Halmashauri ilikuwa na salio la shilingi 4,035,996.91 katika Mifuko yake mbalimbali.

**MAPATO**
Katika Mwezi Disemba 2021, Halmashauri ilikusanya jumla ya shilingi 4,792,628,773.40 Kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoanishwa hapo chini:-



43

| | | |
|---|---|---|
| Mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yenyewe | Tshs. | 1,685,370,874.33 |
| Mapato kutokana na ruzuku ya Mishahara | Tshs. | 1,775,548,130.00 |
| Mapato kutokana na ruzuku ya kawaida | Tshs. | 45,661,416.66 |
| Mapato kutokana na ruzuku ya miradi | Tshs. | 546,767,485.35 |
| Wafadhili | Tshs. | 739,280,867.06 |
| **Jumla ya mapato** (Mwezi Disemba 2021) | **Tshs.** | **4,792,628,773.40** |
| **Jumla ya mapato** na salio la anzia | **Tshs.** | **8,828,093,770.31** |

**MATUMIZI**

Katika kipindi cha Mwezi Disemba 2021, Halmashauri imetumia jumla ya shilingi 4,855,310,946.24 katika maeneo yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya kawaida kutoka vyanzo vya Halmashauri | Tshs. | 453,421,003.12 |
| Matumizi ya Maendeleo vyanzo vya Halmashauri | Tshs. | 867,724,973.10 |
| Matumizi ya Mishahara | Tshs. | 1,775,548,130.00 |
| Matumizi ya Ruzuku ya kawaida | Tshs. | 25,325,500.00 |
| Matumizi ya Miradi ya maendeleo | Tshs. | 960,252,657.22 |
| Wafadhili | Tshs. | 773,038,682.80 |
| **Jumla ya Matumizi** | **Tshs.** | **4,855,310,946.24** |
| Salio mwezi 31 Disemba, 2021 | **Tshs.** | **3,972,782,824.07** |

**SUALA LA BAADHI YA VYANZO VYA MAPATO KUTOONESHA MAKUSANYO**

Iliulizwa kwanini baadhi ya vyanzo vya mapato havionyeshi kiasi cha makusanyo kwa mwezi disemba. Ilijibiwa kuwa vyanzo hivyo havijakusanya ushuru kwa mwezi huu. Aidha, kwa upande wa usafi wa mazingira ushuru ulikusanywa na taarifa ya makusanyo hayo yatawasilshwa katika taarifa ya mwezi januari.

**USHAURI**

Ilishauriwa makusanyo yawe yanawasilishwa ndani ya wiki ya kwanza ya mwezi husika ili yaweze kuonekana kwenye mfumo.

***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**MUHT.NA. 45/2022- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI (OKTOBA - DISEMBA 2021)**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa hiyo ambapo alieleza Mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya Tandahimba iliidhinisha kupokea na kutumia jumla ya Shilingi 13,259,709,918.00 katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa fedha zinazotarajiwa kuchangiwa na wadau mbalimbali ikiwemo Mapato ya ndani ya Halmashauri (OwnSource), Ruzuku kutoka Serikali Kuu, pamoja na Ruzuku kutoka kwa Wafadhili. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2021 (robo ya pili) Halmashauri ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 6,751,328,090.62. Ambapo fedha shilingi 1,850,000,000/= zilitolewa na Serikali kuu kupitia mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO 19 (TCRP) kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi(3 kwa 1) na ujenzi wa vyumba vya madarasa 88 kwa shule za sekondari 82 na shule za msingi( shule shikizi ) 6. hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2021 (robo ya pili) miradi ya vyumba 88 vya madarasa ulikuwa umekamilika na ujenzi wa nyumba ya watumishi ilikuwa hatua ya umaliziaji.

***Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa***

**USHAURI**
Ilishauwa miradi inayoendelea kutekeleza sasa mahitaji ya vifaa vinunuliwe kwa pamoja kutoka kiwandani ili kupunguza gharama.

Katibu aliupokea ushauri na kusema suala la saruji zitanunuliwa katika kiwanda cha Dangote Mtwara na kusisitiza manunuzi mengine yafuate utaratibu na malipo yafanyike baada ya vifaa kufika.

**MUHT.NA. 46/2022- TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI ZA IDARA ROBO YA PILI (OKTOBA – DISEMBA 2021)**

**A. IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Afisa Utumishi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa hiyo ambapo alieleza kazi zilizofanyika katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2021) ni kama ifuatavyo.

I. Kuandaa na kuratibu ratiba za vikao vya Menejimenti na vikao vyote vya kamati za kudumu na kuhakikisha vikao vimefanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni na taratibu za Halmashauri
II. Kuandaa Mishahara ya Watumishi
III. Kushughulikia mikopo ya watumishi kutoka taasisi za fedha.
IV. Kuandaa bajeti ya kawaida ya Idara ya utawala na bajeti ya Mishahara ya watumishi.

***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**B. KITENGO CHA MANUNUZI**

Afisa Manunuzi na Ugavi (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za idara ambapo alieleza kuwa katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2021) ambapo alisema kitengo kiliendelea kufanya kazi zake za manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali kutoka idara mbalimbali kwa kufuata kanuni, taratibu na sheria za manunuzi na kwa kutumia bodi ya zabuni kwa zabuni zilizoridhiwa na bodi. Alisema, kwa robo hii shughuli zilizofanyika ni pamoja na ununuzi wa shajala, samani, manunuzi ya pikipiki za ujenzi na manunuzi wa vifaa vya ujenzi

**TAARIFA YA MAFUTA.**

Katika robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2021) Halmashauri ilifanya manunuzi mafuta Diesel lita 19,130 yenye thamani ya Tsh. 44,632,002,07 na Petroli lita 2310 yenye thamani ya Tsh.5,775,000.00 na kufanya Jumla ya gharama za mafuta kuwa Tsh. 50,407,002.07.00

Iliulizwa pikipiki zilinunuliwa nne (04) kwa ajili ya idara ya ujenzi kwanini idara hiyo zilipewa pikipiki mbili (02). Ilijibiwa kuwa pikipiki moja (01) ipo manunuzi na nyingine ilipelekwa kusaidia shughuli za ulinzi na usalama.
***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**C. KITENGO CHA SHERIA**

Afisa Sheria kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za idara ambapo alieleza kuwa katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2021) kazi zilizotekelezwa ni,

I. Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Halmashauri
II. kuandaa rasimu ya Sheria ndogo kwa Halmashauri
III. Kuhudhuria vikao mbalimbalivya ndani na nje ya Halmashauri
IV. Kutoa ushauri wa kisheria kwa wananchi 24
V. Kuhudhuria Mahakamani kwenye kesi mbalimbali zinazohusu taasisi.
VI. Kusimamia utendaji kazi wa Mabaraza ya Kata.
VII. Kusimamia ukusanywaji wa mapato ya Halmashauri
VIII. Kuandaa mikataba ya ujenzi wa majengo ya taasisi

**MASHAURI YALIYOPO MAHAKAMANI**

1. Shauri la Madai kati ya Halmashauri ya Wilaya Tandahimba na Hamisi Mshamu Mnyuvele na Wenzake 13(57/2017).
2. Shauri la Madai kati ya Hamisi Namkoka dhidi ya Halmashauri ya Kijiji cha Muungano (Land Appeal No. 593/2021).
3. Shauri la Maombi ya kulipwa gharama za kesi baina ya Serikali ya Kijiji cha Muungano na Hamisi Bakari Namkoka (Land Appeal No. 544/2021).

**D. KITENGO CHA TEHAMA**

Afisa TEHAMA (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara ambapo alieleza kuwa katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2021) kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo,

1. Kufanya matengenezo ya kawaida ya vifaa vya TEHAMA katika idara Mbalimbali
2. Kutoa ushauri na kusaidia kiufundi kwa watumiaji wa mifumo katika idara mbalimbali.

**HABARI NA MAHUSIANO YA UMMA**

- Kutoa Habari Mbalimbali za Halmashauri kwenye Tovuti ya Halmashauri na mitandao ya kijamii
- Kuweka taarifa mbalimbali za Halmashauri kwenye mitandao ya kijamii (Instagram na Facebook)
- Kuripoti taarifa mbalimbali kwa kushirikiana na vyombo vya habari vya nje
- Kuandaa Logo stika kwa ajili ya matukio mbalimbali zikiwemo pongezi kwa viongozi wa kitaifa.

***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**MUHT.NA. 47/2022- MPANGO WA MOTISHA WA HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA KWA MWAKA 2022 - 2027**

Kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W) aliwasilisha taarifa hiyo ambapo alisema Kanuni ya 146 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 iliyotungwa chini ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 pamoja na sera ya Taifa ya motisha ya mwaka 2010 zinatoa fursa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka Mpango wa namna ya kutoa motisha mbalimbali kwa watumishi wake kwa kadri inavyoona inafaa. Lengo kubwa la kutoa



46

motisha ni kuwavutia Watumishi kuendelea kufanya kazi katika Halmashauri, kuongeza tija na ari ya kuwatumikia wananchi katika Halmashauri.
Alisema, Uzoefu unaonyesha kuwa mazingira magumu ya kazi na yasiyoridhisha yamesababisha Watumishi wengi kukata tamaa, utoro wa mara kwa mara, kuacha kazi na kwenda mahali pengine kwa ajili ya kutafuta Mazingira bora zaidi na hali hii inasababisha Halmashauri kukosa wataalamu mbalimbali.

Alisema, Ingawa motisha ya fedha bado inaonekana kama ndiyo motisha inayoweza kuwafanya Watumishi kuridhika na kazi zao na Mazingira wanayofanyia kazi, pia kuna motisha ambazo hazihusishi kutolewa fedha zinayo nafasi kubwa katika kutoa motisha kwa Watumishi na kuwafanya waridhike na kazi zao. Kuwashirikisha Watumishi katika maamuzi, kutoa maneno ya pongezi kwa Watumishi wanapofanya vizuri, kutambua mchango wao katika Taasisi/ Idara, mrejesho juu ya utendaji kazi n.k.

**SUALA LA UNUNUZI WA PIKIPIKI KWA AJILI YA OFISI YA WATENDAJI KATA**
Kikao kilisema zinunuliwe pikipiki kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Mtendaji Kata ikiwa kama Motisha na kuwasaidia Watendaji kata katika kukusanya Mapato.

*Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa*

**MUHT.NA. 48/2022- SERA YA MAFUNZO YA HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA YA MWAKA 2020/2021 - 2024/2025.**
Mafunzo kwa watumishi ni kitu muhimu sana kwa ajili ya kuboresha utendaji wa kazi. Aidha, mafunzo ni nyenzo inayotakiwa kutolewa mara kwa mara kwa watumishi ili kuwawezesha kupambana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika ulimwengu. Kwa msingi huu, Waajiri wote wanatakiwa kuandaa utaratibu mzuri utakaowawezesha kuchambua, kutambua, kutoa mafunzo yenye tija kwa watumishi wao na baadae kuwaongezea uwezo wa kuyatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na hivyo malengo ya Taasisi kufikiwa kwa wakati.

Alisema, Sera ya Mafunzo ya Halmashauri ya Wilaya Tandahimba imeandaliwa kwa kuzingatia Sera ya Maboresho ya mwaka 1998, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na Kanuni zake za mwaka 2003 - (Kanuni Namba 103), Waraka wa Utumishi Na.4 wa mwaka 2005: Mafunzo elekezi ya awali kwa watumishi wa Umma, Waraka wenye kumb. Na. DB.307/440/01/B/4 wa tarehe 20 Nov. 2006: Mahitaji na Mipango ya mafunzo kwa Watumishi wa Umma na Waraka wa Elimu Na.9 wa mwaka 2006.

Kikao kilisema mafunzo ni muhimu kwa watumishi lakini wasiruhusiwe wote kwa pamoja kwenda kusoma hasa kwa mafunzo ya muda mrefu ili kazi ziendelee kutekelezeka.

*Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.*

**MUHT.NA. 49/2022- MAOMBI YA KUFUTA KIASI CHA TSH.41,841,033.67 FEDHA ZA MISHAHARA YA WATUMISHI WALIOFARIKI DUNIA**

Afisa Utumishi alisema Halmashauri ya Wilaya Tandahimba katika ukaguzi wa Mishahara uliofanywa na Mkaguzi wa Ndani kwa mwaka 2015 hadi Mwezi Juni, 2020, imebainika kuna mishahara ililipwa kwa watumishi waliostafu kazi, kufariki dunia na kufukuzwa kazi yenye jumla ya Tshs. 166,737,197.38. alisema Tshs. 47,737,197.38 za watumishi waliostaafu zilirejeshwa hivyo aliwasilisha ombi la kufutiwa Tshs.41,841,033.67 za fedha ambazo wanadaiwa watumishi waliofariki dunia ambapo deni hili haliwezi kulipwa kwa sababu wadaiwa hawapo duniani.

Alisema, kwa watumishi waliostaafu ambao bado hawajalipa fedha hizo walishapelekwa polisi ili wachukuliwe hatua za kulipa deni hilo.

**Baada ya majadiliano wajumbe wote kwa pamoja waliridhia kufuta kiasi cha Tsh. 41,841,033.67 fedha za mishahara ya watumishi waliofariki.**

*Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa*

**MUHT.NA. 51/2022- MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

**SUALA LA STAHIKI ZA WATUMISHI**

**Mjumbe alitaka kujua stahiki za watumishi waliostaafu zikoje. Ilijibiwa kuwa mtumishi anapostaafu Halmashauri inalipa gharama za nauli na hela ya kusafirishia mizigo kulingana na mahali anakotoka.**

**MUHT.NA. 51/2022- KUFUNGA KIKAO**

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki kikamilifu katika kikao na kisha alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango na mawazo yao kisha alifunga kikao **Saa 07:23 Mchana.**

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA:**

| | |
|---|---|
| **JINA** ISSA NAMANGA | **JINA** JUMA L. NANGOLOLO |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| **SAINI** [signature] | **SAINI** [signature] |

28/2/2022

**TAREHE**